# Kanuni ya Mwenendo ya Mgawaji

Tume ya Makaburi ya Vita ya Jumuiya ya Madola (CWGC) imekabidhiwa heshima kubwa ya kutunza makaburi, kumbukumbu, rekodi, na masimulizi ya wale kutoka Jumuiya ambao waliokufa wakitoa utumishi, au kama matokeo ya mapambano katika vile Vita viwili vya Ulimwengu.

Sisi ni shirika la utunzaji wa kudumu, ambao unaonyeshwa kila siku, katika yote tunayofanya, katika ~~kile tulicho~~ uwepo wetu, na katika jinsi tunavyofanya kazi. Maadili yetu wenyewe ya CARE yanaonyesha na kuweka utamaduni wetu kama matarajio ya pamoja, tabia, na viwango na tuna matarajio yaleyale kutoka kwa wale wanaofanya kazi pamoja nasi na wanaotufanyia kazi.

Kwa kuingia katika uhusiano na CWGC, tunakuhitaji uzingatie na kufuata sheria zote zinazotumika pamoja na kanuni 8 zifuatazo za mwenendo wa kisheria na maadili:

| | |
|---|---|
| 1. Utaweka hatua madhubuti za kupambana na rushwa na ufisadi.<br><br>Hii inamaanisha kwamba wewe, na wale wanaokufanyia kazi:<br><br>• hutatoa wala kupokea rushwa<br>• hutatoa hongo (kwa mfano, ili kuharakisha huduma au kuepuka udhibiti wa serikali)<br>• utafuata sheria zote za rushwa zinazotumika | 2. Utaepuka mgongano wa masilahi<br><br>Hii inamaanisha kwamba wewe, na wale wanaokufanyia kazi:<br><br>• utaepuka masilahi ya kibinafsi katika kitu chochote kinachofanya iwe vigumu kwako kufanya kazi nyakati zote kwa masilahi bora ya CWGC<br>• utatangaza masilahi yoyote ya kibinafsi au ya kifedha uliyo nayo ambayo yanaweza kuathiri CWGC |
| 3. Hutajihusisha na, wala kuvumilia, aina yoyote ya utumwa au magendo ya binadamu, au matumizi mabaya mengine ya haki za binadamu.<br>Hii inamaanisha kwamba wewe, na wale wanaokufanyia kazi:<br><br>• hutalazimisha watu kufanya kazi kwa vitisho au kutumia watoto<br>• hutatumia watumwa kwa malengo yoyote<br>• hutadhibiti matembezi ya wafanyakazi wako<br>• hutafanya magendo ya binadamu wala kutumia watu ambao wameletwa kimagendo katika shughuli zako<br>• utalipa malipo ya haki wala hutazuilia mshahara<br>• utaweka mikataba ya ajira | 4. Utawatendea wale wanaokufanyia kazi, au unaofanya kazi pamoja nao, kwa usawa, na kwa hadhi na heshima.<br><br>Hii inamaanisha kwamba wewe, na wale wanaokufanyia kazi:<br><br>• hutadhulumu, kunyanyasa au kuwatisha wafanyakazi wako<br>• hutabagua<br>• utawatendea watu kwa haki na usawa bila kujali umri, kabila, rangi, utaifa, dini/imani, jinsia, hali ya ndoa/mwenzi, ujauzito/uzazi, au mwelekeo wa kijinsia<br>• kutimiza sheria husika za usawa na kutobagua |

- utafuata sheria za haki za binadamu

### 5. Utaandaa mazingira salama na yenye afya ya kufanyia kazi.

Hii inamaanisha kwamba wewe, na wale wanaokufanyia kazi:

- utakuwa na ustadi na kufanya mafunzo yanayohitajika
- utahakikisha vifaa vya kazi ni salama, vinadumishwa ifaavyo, vinazingatia sheria, vinatumiwa na kuhifadhiwa kwa usalama
- utafuata miongozo ya afya na usalama inayoandaliwa na CWGC
- utafuata sheria husika ya afya na usalama

### 6. Utalinda mazingira dhidi ya madhara

Hii inamaanisha kwamba wewe, na wale wanaokufanyia kazi:

- utafuata sheria zote za mazingira na ujitahidi kutimiza viwango vya mazoea bora
- utapunguza athari kwa mazingira ya shughuli zako na bidhaa na/au huduma ambazo wewe, na wahusika wako wa nje, huipatia CWGC
- utadhibiti taka kisheria

### 7. Utahakikisha kwamba hakuna bidhaa au vifaa vinapatikana kupitia mazoea haramu au yasiyo ya kiadili.

Hii inamaanisha kwamba wewe, na wale wanaokufanyia kazi:

- hutaisambazia CWGC vifaa au bidhaa zozote kupitia mazoea haramu au yasiyo ya kiadili (na uweze kuthibitisha hii ukiombwa kufanya hivyo)
- hutanunua madini yoyote ya mgogoro

### 8. Utalinda akili mali yetu, data na taarifa ya siri dhidi ya ufikiaji au matumizi yasiyoidhinishwa.

Hii inamaanisha kwamba wewe, na wale wanaokufanyia kazi:

- utahifadhi data ya CWGC kwa usalama na kwa siri
- hutashiriki data ya CWGC bila kibali (ikiwemo kwa makontrakta wako wadogo)
- hutavaa mavazi yenye chapa ya CWGC au kufanya chochote kinachoweza kuonyesha kwamba wewe ni mfanyakazi wa CWGC
- Utafuata sheria zote zinazotumika za ulinzi wa data
- utaripoti masuala yoyote ya usalama wa data au taarifa kwa CWGC mara moja

Tunaweza kukuomba utoe habari za kuthibitisha kwamba unafuata matakwa haya hapo mwanzoni na katika muda wa maisha ya uhusiano wetu wa kazi. Huenda tusifanye au huenda tukakomesha uhusiano na wewe iwapo hutafuata, au huwezi kufuata, matakwa haya.

Tunakuhimiza useme kwa ujasiri kuhusu suala lolote, makosa, au mwenendo usio wa maadili katika sehemu yoyote ya shughuli yetu au mnyororo wa ugavi. Tafadhali tuma barua pepe ya shaka zako kwa: concerns@cwgc.org.

Ikiwa una maswali au maulizo yoyote yanayohusiana na Kanuni hii ya Mwenendo ya Mgawaji, tafadhali mweleze mwasiliani wako wa CWGC au utume barua pepe kwa Timu ya Uzingatiaji ya CWGC moja kwa moja ~~kwenda~~ kupitia; compliance.ethics@cwgc.org.

## Udhibiti wa Toleo

| Jina la Hati | Kanuni ya Mwenendo ya Mgawaji (Ukurasa Mmoja) | |
|---|---|---|
| Toleo | 1.0 | |
| Mmiliki wa Hati | Tarehe ya Kutumika | Tarehe ya Mapitio |
| Wakili Mkuu | 01/12/2023 | 01/12/2025 |